THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/2 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2**
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 2:30** **Jumatano, 11 Novemba 2015 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D.
2. Jibu maswali **manne (4)**, swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.


Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

**BISMILLAHIR – RAHMANIR - RAHIIM**

## SEHEMU A: QUR'AN

1. Jadili hoja nne zitolewazo na makafiri wakimsingizia Mtume Muhammad (s.a.w) kuitunga Qur'an kwa manufaa yake binafsi na kabila lake.

2. Andika tafsiri ya Suratu dh-Dhuha na kisha eleza mafunzo sita yatokanayo na Sura hiyo.

3. *Hakika sisi tumeiteremsha Qur'an kwa Kiarabu ili mpate kufahamu (12:2).* Kwa mujibu wa Qur'an, eleza hekima sita za Qur'an kushushwa katika lugha ya Kiarabu.

## SEHEMU B: TAWHIID

4. Kwa kuzingatia kazi sita za Malaika, eleza jinsi imani juu ya kuwepo kwao inavyoathiri maisha ya kila siku ya mwanadamu.

5. Hapana Mtume baada ya Muhammad (s.a.w). Thibitisha kwa kutoa hoja tano.

6. *Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishwa; na Husamehe yasiyokuwa haya kwa Amtakaye. Na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu bila shaka amebuni dhambi kubwa (4:48).* Eleza aina kuu nne za shirk kisha onesha madhara matatu ya shirk kwa mujibu wa Qur'an.

## SEHEMU C: FIQH

7. Ainisha idadi ya rakaa katika swala tano za kila siku, kisha chambua umuhimu wa kusimamisha swala katika Uislamu kwa kutoa hoja sita.

8. *"Na katika ishara zake (za kuonesha Ihsani zake juu yenu) ni kuwa amekuumbieni wake zenu katika jinsi yenu ili mpate utulivu kwao, naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu (30:21).* Fafanua mambo sita ambayo ni wajibu kwa mume kumfanyia mkewe.

9. Kuna aina kuu mbili za talaka, talaka rejea na talaka isiyorejea. Fafanua aina tano za talaka isiyorejea.

## SEHEMU D: TAREKH

10. Chambua mafunzo sita tunayoyapata kutokana na vita vya pili vikubwa alivyoshiriki Mtume (s.a.w).

11. Kwa kurejea historia ya dola ya Kiislamu baada ya kutawafu Mtume (s.a.w) hadi Makhalifa wanne waongofu, eleza njia tatu za kumpata Khalifa kisha bainisha majukumu manne ya Khalifa.

12. Eleza mambo sita yanayodhihirisha uadui wa wanafiki dhidi ya dola ya Kiislamu Madinah.



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner